**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**

**MKOA WA MARA**
Simu Na: 028-2620780
Barua Pepel: barua@musomarrh.go.tz
Tovuti:www.musomarrh.go.tz

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ,
Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere,
S.L.P 21,
**MUSOMA.**

09 Agosti, 2026
**MUSOMA.**

## TAARIFA KWA UMMA

## UFAFANUZI WA MALALAMIKO YA MATIBABU YA NDG. WARIOBA JOSEPH BUTIKU HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA YA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE (KWANGWA)

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere imeona malalamiko ya matibabu ya Ndg. Warioba Joseph Butiku kupitia mitandao ya kijamii. Hospitali inakiri kumpokea mgonjwa huyu mnamo tarehe 7/8/2026 saa moja usiku akiwa ni mgonjwa wa Rufaa kutoka hospitali ya wilaya ya Butiama kwa ajili ya matibabu zaidi. Alipokelewa na kuanzishiwa matibabu ya awali katika Idara ya Dharura na Ajali, baada ya uchunguzi wa kimatibabu mgonjwa huyu alihamishiwa kuendelea na huduma kwenye chumba cha wagonjwa mahututi (ICU) ambapo anaendelea na huduma hiyo mpaka sasa.

Gharama za matibabu ya mgonjwa zimelipwa kwa mujibu wa taratibu za malipo ya Serikali na sehemu nyingine zimetolewa kwa njia ya msamaha wa muda. Kufuatia malalamiko ya ndugu wa mgonjwa kuombwa 150,000/= kwa ajili ya mashine ya kumsaidia mgonjwa kupumua (Mechanical Ventilator) ambayo ni kinyume na taratibu kwani huduma hiyo hailipiwi, Uongozi wa hospitali umechukua hatua zifuatazo:

Yamefanyika mahojiano na ndugu wa mgonjwa kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa na kumtambua mtumishi aliehusika na tukio hili, ambaye atachukuliwa hatua kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za Utumishi wa Umma na zile za kitaaluma. Aidha tukio hili limeripotiwa kwenye Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kwa ajili ya uchunguzi na hatua zaidi.

**MUHIMU:** Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere tunaendelea kuwakumbusha wagonjwa na ndugu wa wagonjwa kuwa malipo yote yanafanyika kwenye dirisha la malipo kupitia namba ya malipo (Control Number) tu. Endapo utapata changamoto usisite kuwasiliana na uongozi wa hospitali kwa namba zilizowekwa kwenye matangazo na zinazoonekana kwenye runinga hospitalini hapa.

**Imetolewa na;**

**Judith Vincent Machumu**

**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kwa Umma**

**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA YA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE**